# Lugha za Kienyeji kama Kizingiti cha Kuleta Umoja wa Kitaifa na Uwiano Barani Afrika

*Basilio Gichobi Mungania*
*Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya*

**Ikisiri**

**Lugha ni chombo muhimu sana katika kuleta umoja na mshikamano wa kitaifa na wa kieneo. Katika taifa la Kenya na kanda ya Afrika ya Mashariki, hakuna lugha iliyo na uwezo wa kuleta mshikamano na muungano tunaoutamani isipokuwa Kiswahili. Kiswahili kina wajibu mkubwa wa kuchangia mshikamano wa kitaifa na wa kikanda. Hata hivyo, lugha hii inakumbwa na changamoto nyingi katika kutekeleza wajibu huu adimu, zikiwemo zile za kijamii, kiuchumi, na za kisiasa. Mojawapo ya changamoto kubwa inatokana na lugha za kiasili ambazo huwa ni kikwazo kikubwa kutokana na kutumiwa kwazo na wananchi wengi katika mataifa mengi ya Afrika ya Mashariki. Lugha za kiasili hutumiwa kwa wingi sana katika mataifa mengi ya Afrika ya Mashariki, hususan katika nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi. Ni katika nchi ya Tanzania pekee ambapo Kiswahili hutumiwa ipasavyo na ndiposa nchi hiyo inaakisi muungano wa kitaifa. Makala haya yatatathmini jinsi lugha ya Kiswahili inavyoweza kutumiwa kama wenzo wa kuchangia katika kujenga umoja na mshikamano wa kitaifa na wa kikanda pamoja na changamoto zinazokikumba Kiswahili katika wajibu wake wa kuleta umoja wa kitaifa na wa kikanda. Zaidi itachanganua ushindani unaotokana na lugha enyeji.**

**Maneno Muhimu:** Lugha Enyeji, Lugha Rasmi, Lugha ya Taifa, Lugha Mawasiliano.

## Utangulizi

Tangu nchi za Kiafrika kujinyakulia uhuru, juhudi nyingi zimefanywa kuweza kuamulia masuala ya lugha na maendeleo ya mataifa husika. Jambo mojawapo ambalo mataifa hayo yameafikiana nalo ni kuwa kunahitajika lugha moja ambayo inaweza kutumiwa kuwasiliana na kuhamasisha wananchi katika juhudi za ujenzi wa taifa. Mataifa mengi ya Afrika, hata hivyo, yana wingi lugha, jambo ambalo linatatiza uchaguzi wa lugha itakayotumiwa kwa minajili ya shughuli za kitaifa na zilizo rasmi. Kwa bahati nzuri, mataifa ya Afrika Mashariki yana lugha inayokubalika na wananchi wengi; lugha isiyohusishwa na unyanyasaji wa jamii

yoyote ile barani Afrika, imetokea kuwa Kiswahili. Lugha hii imewahi kuungwa mkono na wengi kama lugha ya Afrika Mashariki na vilevile lugha ya bara zima la Afrika. Ni hivi majuzi tu ambapo kiongozi wa chama cha EFF kule Afrika Kusini, Bw. Julius Malema alipendekeza Kiswahili kitumiwe kama lugha ya bara la Afrika. Kabla ya hapo, waandishi mashuhuri barani Afrika, kama vile Wole Soyinka miaka ya sitini (kama inavyonukuliwa katika Mulokozi, 2002) na Ayi Kwei Armah (1985), wakiongozwa na mihemko ya Upanafrika pia waliwahi kuunga mkono matumizi ya Kiswahili kama lugha ya bara la Afrika. Licha ya kuungwa mkono na viongozi na wasomi wengi barani Afrika na pia kutambuliwa kama lugha ya Umoja wa Afrika, Kiswahili kingali kinatumika kama lugha ya bara la Afrika. Makala haya yanahoji kuwa lugha enyeji za Afrika huwa ni kizingiti katika kukubalika na kukuzwa kwa Kiswahili kama lugha rasmi na lugha ya taifa.

**Lugha**

Inakisiwa kuwa idadi ya lugha ulimwenguni ni kati ya 6,000 na 7,000. Kati ya lugha hizi ni Kiswahili, ambacho hutumiwa na watu wapatao milioni mia moja ulimwenguni. Katika bara la Afrika, inakisiwa kuwa na idadi ifuatayo ya watu wsanaozungumza Kiswahili (Mulokozi, 2002):

| Nchi | Idadi ya Wazungumzaji |
|---|---|
| Tanzania | 32,000,000 |
| Kenya | 20,000,000 |
| Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 15,000,000 |
| Uganda | 8,000,000 |
| Burundi | 2,000,000 |
| Rwanda | 2,000,000 |
| Mataifa mengine | 1,000,000 |
| Jumla | 80,000,000 |

Lugha ni kifaa au chombo kinachotumiwa ili kukuza mawasiliano na mwingiliano wa kijamii na uwiano wa kitaifa, na uhifadhi wa utamaduni na kwa hivyo kila mtoto ana jukumu la kujifunza lugha inayotumiwa katika mazingira anamoishi.Licha ya kuwa binadamu wana mambo na vifaa vingi vinavyoweza kuwatambulisha, lugha huwa ni kifaa muhimu cha utambulisho na cha kuiunganisha jamii. Kiango (2002) na Mulokozi (2000) wanatambua umuhimu wa lugha kama kitambulisho na kiunganishi cha jamii. Jamii nyingi barani Afrika hukosa kitambulisho halisi kinachoweza kuwaunganisha. Endapo watu hawana lugha inayotumiwa na kueleweka na wazungumzaji wote, itakuwa ni vigumu kwao kuungana katika juhudi za aina yoyote ile za maendeleo. Ili kuweko na

umoja wa kitaifa, ni sharti kuweko na lugha itakayowawezesha kueleanwa. Tatizo mojawapo linalozikabili nchi za Kiafrika ni kuweko kwa wingi lugha katika mataifa husika. Kwa mfano, nchini Tanzania, kunapatikana zaidi ya lugha 120 ilhali nchini Kenya kuna lugha zaidi ya arobaini. Ikiwa wananchi hawana lugha inayoweza kuwaleta pamoja, inakuwa ni vigumu kwao kuungana katika ujenzi wa umoja wa kitaifa. Kila kabila litakuwa likijihisi kama taifa lililo tofauti na jingine[1]. Mtagusano wa lugha enyeji na tamaduni tofautitofauti huchangia pakubwa upatanisho wa lugha na mawasiliano kati ya tamaduni mbalimbali. Wingi lugha hufanya suala la upangaji lugha kuwa gumu zaidi. Mulokozi (2000), akinakiliwa na Kiango (2002:189), amezigawa nchi za Afrika katika makundi yafuatayo kwa kuzingatia lugha:

i) Nchi zenye lugha moja,
ii) Nchi zenye lugha mbili au zaidi lakini zenye lugha kuu kadhaa za kikanda/lugha mawasiliano (lingua franka),
iii) Nchi zenye lugha nyingi lakini zenye lugha mawasiliano moja au mbili za wenyeji, na
iv) Nchi zenye lugha nyingi ambazo hazina lugha mawasiliano au lugha ya kikanda inayozungumzwa na watu wengi.

Nchi za Afrika Mashariki zinaweza kuainishwa ama katika kundi la pili au la tatu ambapo kila nchi ina lugha nyingi za kienyeji ingawaje lugha ya Kiswahili ndiyo inayotumiwa kama lugha mawasiliano baina ya watu kutoka jamii tofautitofauti.

**Lugha, Mawasiliano na Uwiano wa Kitaifa**

Mojawapo ya matatizo yaliyoyakumba mataifa ya Afrika yalipojipatia uhuru ni kuchagua lugha itakayokubalika na raia wote wa nchi husika. Uchaguzi usiofaa na kuungwa mkono na walio wengi ungesababisha vurugu la kisiasa ambalo lingekuwa tisho kubwa kwa mataifa machanga. Uchaguzi mwafaka ulifaa kuongozwa na mambo yafuatayo: iwe lugha isiyoruhusu na kutilia maanani migogoro ya kikabila huku ikilikubalia taifa kuendelea kushiriki katika ujenzi wa jamii ya kimataifa kupitia sayansi, teknolojia, biashara na diplomasia, na

[1] Katika Kenya, ambapo kila jamii hujihisi kama taifa tofauti na jamii nyingine, tumeshuhudia machafuko ya kijamii mara kadhaa baada ya uchaguzi, jambo linalotiliwa mkazo na utaifa wa kijamii. Utaifa huu unasababishwa sana na hisia za wanajamii ambazo huchochewa zaidi na matumizi ya lugha za kienyeji. Jambo hili pia latokana na historia ya ukoloni nchini Kenya ambapo watawala wa kikoloni walisisitiza sera ya "utengano" (maana yake, tenga na utawale)

uchaguzi wa lugha usiwe unaweza kusababisha kutengwa kwa jamii zilizotumia lugha zingine, jambo ambalo sio tofauti na matumizi ya lugha ya kigeni. Mambo haya ndiyo yalikuwa kizingiti kikubwa kwa serikali nyingi barani Afrika kuhusiana na uchaguzi wa lugha ya taifa au lugha rasmi. Ili kulishughulikia suala hili kikamilifu, ni vyema tuelewe fika kuwa kuna uhusiano wa karibu sana kati ya lugha na ujenzi wa uwiano wa kitaifa na kikanda.

Lugha ni chombo cha utambulisho wa kitaifa. Wananchi wanapojitambulisha na taifa, pana uwezekano mkubwa wao kuungana na kushiriki zaidi katika juhudi za kimaendeleo na hivyo basi, kuharakisha maendeleo ya taifa. Jambo hili linawezekana tu ikiwa wananchi wote wa taifa wanatumia lugha moja. Mataifa mengi ambayo yameendelea yalifanikiwa kuchagua lugha ambayo hutumiwa katika shughuli za kimaendeleo. Kutokana na mataifa mengi yanayoendelea kushindwa kuteua lugha itakayotumiwa ama kama lugha rasmi au lugha ya taifa, baadhi ya watalaam wamedai na baadhi ya wataalam kuwa kuna uhusiano wa karibu sana kati ya wingi lugha na ukosefu wa maendeleo. Suala tunaloweza kuuliza hapa ni je, wingi lugha huchangia utengano wa kijamii na kuathiri ustawi wa nchi? Jambo lisilokanushika ni kuwa utengano wa jamii kupitia lugha huzuia vitega uchumi nao wingi lugha na utengano wa kijamii huongeza uwezekano wa vita vya wenyewe kwa wenyewe[2].Matamshi ya chuki hutumiwa na wanasiasa kuhamasisha vijana ili kuwafanya wang'ang'anie ukabila na lugha zao, jambo linalowachochea kujihusisha na vita vya kikabila. Hapa nchini Kenya, kuna mifano kadhaa inayoweza kutolewa kuhusiana na madhara ya matamshi ya uchochezi yatolewayo na wanasiasa, hasa wakati wa kampeni za uchaguzi:

a. Vita vya kuwafurusha watu kutoka maeneo ya bara huko Likoni mwaka wa 1992,
b. Vita vya kuwafurusha watu kutoka eneo la Molo mwaka wa 1997,
c. Vyombo vya habari kuchangia katika kuleta utengano wakati wa kura ya maamuzi ya mwaka 2005,
d. Vita vya baada ya uchaguzi wa mwaka 2007, na
e. Machafuko ya baada ya uchaguzi wa mwaka 2017.

Suala la uwiano na mshikamano lilikuwa muhimu baada ya Kenya kujinyakulia uhuru, jambo lililopelekea nchi kutaka kujitambulisha kama taifa lililojikomboa kutoka minyororo ya kikoloni. Tangu uhuru, juhudi za kujenga mshikamano zimekuwa zikifanywa kila wakati lakini hazijafua dafu bado.

---

[2] Rejelea matukio yaliyotokea Rwanda mwaka 1994 na chuki na mauaji *(Xenophoic attacks)* yaliyofuata baada ya matamshi ya chuki kutolewa na mfalme wa Wazulu Afrika Kusini mwaka 2015.

### Mambo yanayokifanya Kiswahili kufaa kama Lugha ya kuleta Uwiano na Mshikamano

Kati ya lugha zote za Kiafrika, ni Kiswahili pekee ambacho kinapendelewa na kukubaliwa na wengi kama lugha inayoweza kuleta uwiano na mshikamano. Kuna sababu nyingi zinazokipelekea Kiswahili kuungwa mkono kama lugha faafu ya kuleta uwiano na mshikamano. Kwanza kabisa, Kiswahili kimetambuliwa na wataalamu mbalimbali kama lugha inayoweza kutambulisha Waafrika kimataifa. Wataalamu kama vile Wole Soyinka na Ayi Kwei Armah wamekiunga mkono kama lugha ya Kiafrika ambayo inafaa kutumika katika majopo ya Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kutishia kutohudhuria mikutano ya Umoja wa Mataifa iwapo Kiswahili hakingetambuliwa kama mojawapo ya lugha rasmi za Umoja wa Mataifa. Kwa hivyo matumizi ya lugha ya Kiswahili yanakubalika na wengi kama lugha inayoweza kuwatambulisha Wafrika kimataifa.

Pili, Kiswahili ni lugha ambayo inafundishwa katika vyuo vikuu vingi ulimwenguni. Kiswahili kinafundishwa katika vyuo vikuu kama vile vya Bayreuth (Ujerumani), Yale (Marekani), Nanjin (Uchina), na kwingineko. Hivi majuzi, serikali za Afrika Kusini na ile ya Zimbabwe zimekwisha kukubali kukifunza Kiswahili katika shule za humo nchini. Matukio haya ni ya kuridhisha na yanadhihirisha Kiswahili kuwa lugha mashuhuri ya bara zima la Afrika. Jambo hili linaonyesha kuwa Kiswahili kimeshavuka mipaka ya kikabila, kitaifa, kikanda na kimataifa na kinaweza kuchukuliwa kuwa lugha ya kimataifa ambayo inaweza kutumiwa kuleta uwiano na mshikamano barani Afrika. Kiswahili kinaweza kutumiwa kama kitambulisho cha watu wanaokitumia ulimwenguni na kuwafanya wajione kama kitu kimoja na walio na lengo moja.

Kiswahili kinatumika kama kitambulisho cha utamaduni, utamaduni ambao umeenea kote ulimwenguni. Wanamuziki wengi katika kanda ya Afrika Mashariki hutumia lugha ya Kiswahili katika nyimbo zao, nyimbo ambazo zinasaidia kukieneza Kiswahili popote ulimwenguni. Waimbaji kama vile Miriam Makeba na Yvonne Chaka wa Afrika Kusini wamewahi kutumia Kiswahili katika nyimbo zao, jambo linalothibitisha kuwa Kiswahili sio lugha ya wenyeji wa Afrika Mashariki peke yao. Kadhalika, kuna michezo ya kuigiza au drama ambazo huigizwa kwa Kiswahili na kuchangia katika kukisambaza Kiswahili ulimwenguni. Pia tusisahau wanaspoti ambao wameziletea nchi zetu sifa nyingi. Wengi wa wanamichezo hawa huwa wanasaidia kukisambaza Kiswahili ulimwenguni wanaposhindana na watu kutoka mataifa mbalimbali. Wanaspoti kutoka nje pia huja huku kwetu kufanya mazoezi na wanaspoti wa hapa kwetu ambapo wanafanya mazoezi kwa pamoja katika vituo vya mafunzo na majaribio vya hapa petu. Utamaduni pendwa unasaidia kueneza Kiswahili kupitia kwa kazi za kubuni, drama, na muziki.

Hatimaye, viongozi wa mataifa ya Afrika Mashariki wamesaidia katika kukipiga jeki Kiswahili. Kupitia kwa Umoja wa Afrika Mashariki, kumeundwa kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki, kamisheni ambayo inalenga kusaidia kueneza matumizi ya Kiswahili katika mataifa wanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki. Hatua hii imekifanya Kiswahili kikawa somo linalofundishwa katika mataifa wanachama. Kwa hivyo, Kiswahili kinatumika kama chombo cha kuleta umoja na uwiano kati ya mataifa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Changamoto za Kiswahili kama Lugha ya kuleta Uwiano na Mshikamano**

Ingawa Kiswahili kinafaa kutumiwa ili kuleta uwiano na mshikamano, kinakumbwa na changamoto nyingi. Katika sehemu hii, nitashughulikia baadhi ya matatizo yanayokikumba Kiswahili kama wenzo wa kuleta uwiano na mshikamano nchini, katika kanda, na barani Afrika.

Mojawapo ya sababu zinazokikumba Kiswahili ni zile za kiuchumi. Jamii ya Waswahili haina kundi lenye uwezo wa kiuchumi linaloweza kupigia upatu lugha ya Kiswahili itumike kama lugha mawasiliano na lugha rasmi barani Afrika. Makundi yenye uwezo wa kiuchumi huwa yanaunga mkono ukuzaji wa lugha za kigeni kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, na hivi majuzi Kichina. Lugha hizi za kigeni huungwa mkono na serikali za mataifa ambapo lugha hizo hutumiwa kama lugha za kwanza na huwa kuna mashirika ya kiserikali ambayo jukumu lake ni kukuza lugha hizoLugha hizi za kigeni zinaungwa mkono na kufadhiliwa na serikali za nje kupitia mashirika yao ya kukuza lugha hizo[3].Lugha sio tu kifaa cha mawasiliano bali pia huamulia masuala ya kisiasa na itikadi za jamii. Lugha inavyotumiwa kuwasiliana huchangia kuleta tofauti za kijamii na kisiasa. Ukuzaji wa lugha hizi pamoja na kuwa serikali zetu hazina mashirika ya kukuza lugha ya Kiswahili bila shaka kunakinyima Kiswahili nafasi ya kukua kama lugha ya mawasiliano mapana ili iweze kutumiwa kuleta uwiano na mshikamano barani Afrika.

Kiswahili pia hukumbwa na matatizo ya kisheria. Licha ya kuwa Kiswahili kimetambuliwa kama lugha rasmi na lugha ya taifa nchini Kenya (ibara ya 7 ya katiba ya Kenya ya mwaka 2010), hakuna juhudi ambazo zimefanywa kisheria kuhakikisha kuwa lugha hii inapewa msukumo wa kisheria. Hakuna sheria yoyote iliyopitishwa na bunge la Kenya kukifanya Kiswahili kitambuliwe kisheria kama lugha rasmi au lugha ya taifa. Hivi majuzi baraza la mawaziri limekubali

[3] Tazama mashirika kama vile British Council ambayo hukuza Kiingereza, Alliance Francais ambayo hukuza Kifaransa, Goethe Institute inayokuza Kijerumani, na Confucius Institute inayokuza Kichina.

kuundwa kwa baraza la Kiswahili ambalo litakuwa na jukumu la kukikuza Kiswahili nchini Kenya kulingana na itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tunatumaini kuwa juhudi hizi hazitalemazwa na msukumo huu utaendelezwa kwa udi na uvumba.

Kiswahili na upanafrika ni suala ambalo pia halijawahi kutiliwa mkazo kisheria. Licha ya kuungwa mkono na wasomi mashuhuri barani Afrika (Wole Soyinka miaka ya sitini na Ayi Kwei Armah miaka ya themanini), Kiswahili hakijafanyiwa juhudi za kukikuza kama lugha ya bara zima la Afrika. Katiba ya Kenya ya mwaka 2010, ibara ya 35 inazungumzia haki za kibinadamu na wananchi. Kila mwananchi ana haki ya kupokea habari anazozihitaji maadam ziwe hazikinzani na zile za watu wengine. Licha ya uhuru huu wa kikatiba, kuna sheria zingine chungu nzima ambazo zinawazuia wanahabari kutekeleza kazi zao ipasavyo, kwa mfano, sheria ya kumharibia mtu jina *(Defamation law)*, sheria ya kukashifu kimaandishi *(libel)*, na sheria ya habari na mawasiliano *(Information and communication Act, 1998)*, na nyinginezo. Kadhalika, Kiswahili hukumbwa na ushindani kutoka lugha enyeji. Baadhi ya vituo vya utangazaji vinavyotumia lugha enyeji vilichangia pakubwa kuenea kwa chuki kati ya jamii mbalimbali nchini Kenya baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007. Mchango wa lugha enyeji katika kukitinga Kiswahili utajadiliwa kwa mapana katika sehemu zinazofuatia.

Kiswahili pia hukumbwa na changamoto za teknolojia na utandawazi. Sote tunakubaliana kuwa wepesi wa mabadiliko ya sayansi na teknolojia unakipelekea Kiswahili kuhitajika kupiga hatua za kujiendeleza kwa kasi mno. Hatua hizi haziwezekani ikiwa serikali zetu hazitakitengea pesa za kufadhili ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Kila wakati pesa zinapohitajika kwa minajili ya ukuzaji wa Kiswahili, udhuru unaotolewa ni kwamba hakuna pesa za kufadhili majukumu hayo. Teknolojia ni ghali na iwapo twataka kuwamo katika mchakato wa mabadiliko ya kiteknolojia hatuna budi kujitolea kwa hali na mali kugharamia maendeleo ya Kiswahili ili kiweze kukidhi mahitaji ya karne ya 21.

### Lugha, Siasa, Uwiano na Mshikamano wa Kitaifa

Wanasiasa hutumia semi za chuki zinazolenga kuchochea uhasama kati ya jamii tofautitofauti na hivyo basi kuendeleza ajenda zao za kibinafsi na za kisiasa. Semi hizi aghalabu hutolewa kwa lugha za kienyeji. Jamii za Kenya huishi kwa amani sikuzote isipokuwa wakati wa uchaguzi kila baada ya miaka mitano wakati ambapo hotuba za wanasiasa hutoa matamshi ya chuki ambayo huwachochea dhidi ya wenzao kutoka makabila mengine. Wakenya hujihisi kama wanajamii

wa makabila yao[4]. Ujenzi wa utaifa kwa watu wanaojihisi kama wanajamii wa kabila fulani huwa ni suala zito sana. Kadhalika, wanasiasa wameekeza katika vyombo vya habari na huvitumia vyombo hivyo kuendeleza maslahi yao, jambo linalohatarisha demokrasia na mahitaji ya wanahabari kuwa huru.

Wanasiasa daima hulenga kujijenga kibinafsi kuanzia kwa wanajamii wao. Kila mwanasiasa hujaribu iwezekanavyo kuwaleta watu wa kabila lake chini ya himaya yake ilimradi wawe wanamuenzi yeye tu. Vyombo hivyo vimetumiwa pakubwa kueneza jumbe za chuki ambazo zimechangia kuchochea uhasama kati ya jamii tofautitofauti katika nchi. Vyombo vinavyomilikiwa na jamii sio tofauti na vile vinavyomilikiwa na wanasiasa kwa vile huwa vinaendeshwa na kusimamiwa vibaya hivyo basi kuweza kutumiwa vibaya na wanasiasa wa kutoka jamii husika. Tazama madhara ya matamshi ya chuki ya wanasiasa kutokana na vyombo vya habari kuegemea upande mmoja wa kisiasa na kuchochea uhasama kati ya wanajamii husika:

i) Vita vya kuwafurusha watu kutoka maeneo ya bara huko Likoni kabla ya uchaguzi wa mwaka 1992,
ii) Vita vya kuwafurusha watu wa jamii fulani kutoka Molo mwaka wa 1997,
iii) Vyombo vya habari kuchangia katika kuleta utengano wakati wa kura ya maamuzi ya katiba mpya mwaka 2005,
iv) Vita vya baada ya uchaguzi wa mwaka 2007,
v) Chuki na mauaji yaliyofuata baada ya matamshi ya chuki kutolewa na mfalme wa Wazulu huko Afrika Kusini mnamo 2015, na
vi) Vyombo vya habari kuchangia vurugu baada ya uchaguzi wa mwaka 2107.

Suala la uwiano na mshikamano lilikuwa muhimu sana baada ya Kenya kujinyakulia uhuru, jambo lililopelekea nchi kutaka kujitambulisha kama taifa lililojikomboa kutoka minyororo ya kikoloni. Tangu uhuru, juhudi za kujenga mshikamano zimekuwa zikifanywa kila wakati lakini hazijafua dafu bado. Wanahabari wa humu nchini hawana uwezo wa kukusanya na kusambaza habari zinazohusiana na uhasama. Wamiliki wa vyombo vya habari na wasimamizi wa vyombo hivi huathiri kimaamuzi yale yanayopatikana katika vyombo hivi kwa

[4] Mizizi ya kikabila nchini Kenya ilipandwa na wakoloni wa Kiingereza ambao waliendeleza utawala wa Kiingereza uliojulikana kama "Gawanya Utawale" ambao ulisisitiza ukabila na matumizi ya lugha za kikabila, tofauti na ule ulioendelezwa na Wajerumani kule Tanzania ambao ulisisitiza matumizi ya Kiswahili.

njia mbalimbali; wanaweza kufanikisha utendakazi wa vyombo vya habari kutekeleza majukumu yao kwa njia zifuatazo:

a) Kuwaajiri wanahabari walio na mwelekeo na mtazamo ulio sawa na wao,
b) Kuwateua watu walio na mwegemeo/mtazamo kama wao katika nyadhifa mbalimbali za uongozi katika makampuni yao,
c) Kuunga mkono kuchaguliwa kwa watu walio na mtazamo ulio sawa na wao katika nyadhifa za kitaifa, na
d) Kuunga mkono sheria na kanuni zitakazosaidia kukuza biashara zao.

Njia hizi zote zinaweza kuathiri pakubwa uamili wa Kiswahili kama chombo cha kuleta uwiano na mshikamano wa kitaifa. Endapo wanahabari hawatakuwa huru kuendesha kazi zao ipasavyo na badala yake wawe wanaendeleza maslahi ya waajiri wao (ambao huenda hawatilii maanani maslahi ya jamii), basi uhasama utadumu baina ya jamii husika.

Uhasama wa kisiasa aghalabu hutokana na mitafaruku yenye misingi yake katika utambulisho wa kikabila na dhuluma za kihistoria. Tukilinganisha utawala wa Moi na ule wa Kibaki nchini Kenya tunaweza kugundua namna wanasiasa wanavyotumia uwezo wao wa kisiasa kuleta au kuvuruga uwiano na mshikamano. Katika awamu ya kwanza ya utawala wa Moi, vyombo vya habari vililenga kuhifadhi maslahi yavyo ya kibiashara na hivyo basi habari nyingi zilikuwa za kimaendeleo. Lakini katika awamu ya pili, Kenya iliingia katika mfumo wa vyama vingi na upanuzi wa vyombo vya habari. Wakati huu, vyombo vya habari vilijaribu kuunga mkono mabadiliko ya kisiasa. Katika mwaka wa 1996, vituo vya kutangazia vya Capital FM (redio) na KTN (televisheni), ambavyo vilimilikiwa na Baraza Ltd chini ya kampuni ya Standard vilianzishwa. Baada ya kuanzishwa kwa vituo hivi, idhaa zingine zikafuatia, kama vile Royal media Group, na vinginevyo.

Ikumbukwe kwamba, wakati huo, utoaji wa leseni, kwa kiasi kikubwa, ulitegemea msimamo wa kisiasa wa mmiliki. Kwa mfano, wakati S. K. Macharia (mmiliki wa Royal Media Group inayomiliki vituo vingi vya utangazaji) alipoanza kushirikiana na Mwai Kibaki, ambaye alikuwa kiongozi wa upinzani wakati huo, leseni zake zilitwaliwa na serikali. Lakini alipotangaza kujitenga na Kibaki na kuunda kikundi cha wanamaendeleo kutoka mkoa wa Kati, alirudishiwa leseni zake. Vituo vya awali vilivyoanzishwa vilikuwa vikitangaza kwa ama Kiingereza au Kiswahili, jambo ambalo liliwatenga Wakenya wengi ambao hawakuwa na ujuzi wa lugha hizo.

Kuanzishwa kwa vituo vya kutangazia kwa lugha za kienyeji kulianza mwaka wa 2000. Idhaa ya kutangazia kwa lugha ya Kikikuyu ya Kameme FM, kituo cha kwanza kutangaza kwa kutumia lugha ya kienyeji, ilianzishwa. Ufanisi wa Kameme FM kulipelekea idhaa zingine kufunguliwa zilizotangaza kwa lugha

enyeji: Ramogi FM (Wajaluo), Kass FM (Wakalenjin), Egesa FM (Wakisii), Musyi FM (Wakamba), Mulembe FM (Waluhya), na vingine vingi. Vituo hivi vililenga jamii maalum. Vipindi vya mazungumzo (hasa asubuhi) vililenga kuamsha hisia za kikabila ili kumaliza upinzani. Vita vingi vilivyoshuhudiwa na ambavyo vingali vikishuhudiwa kila tunapokaribia uchaguzi husababishwa na matangazo yanayosambazwa kupitia vituo hivi vinavyotumia lugha za kienyeji, jambo ambalo linakuwa tisho kwa Kiswahili kama wenzo wa kuleta umoja na mshikamano katika Kenya.

Wakati wa utawala wa Kibaki, umiliki wa nguvu za utawala ulionekana kuwa ni wa ama kuwamo *(inclusion)* au kutokuwemo *(exclusion)*. Upanuzi wa vyombo vya habari wakati huu haukuambatana na uwekaji wa sera mwafaka za kusimamia utangazaji. Vituo vya utangazaji vilikuwa na misimamo ya kisiasa iliyoegemea upande fulani wa kisiasa huku vikisisitiza maslahi ya kijamii. Watangazaji wengi walipewa kazi katika vituo vya utangazaji kutokana na uwezo wao wa kutumia lugha enyeji bila kujali ustadi na ujuzi wao wa kikazi. Watangazaji hawakuwa na utaalam wowote au masomo ya uanahabari; wengi wao walipewa kazi kutokana na uwezo wao wa kuchekesha au/na kuigiza. Ukosefu wa ustadi wa uanahabari ulijitokeza zaidi katika vipindi vya majadiliano pale wanahabari waliposhindwa kuongoza na kuthibiti mijadala. Semi zilizotolewa na kusambazwa kupitia vituo vya utangazaji zilichangia pakubwa kupanda mbegu ya uhasama wa kikabila kati ya jamii mbalimbali za Kenya. Hadi kufikia leo, mbegu zilizopandwa zingali zinatutinga na kuathiri umoja, uwiano na mshikamano wa kitaifa.

**Vyombo vya Habari, Lugha, Uwiano na Mshikamano wa Kitaifa**

Vyombo vya habari vina uwezo mkubwa wa kukisambaza na kukieneza Kiswahili katika kila pembe ya dunia kwa haraka sana kupitia magazeti, redio, televisheni, na vyombo vinginevyo.Lugha ni chombo muhimu sana cha kuleta mshikamano wa kitaifa, kikanda, na bara zima la Afrika. Vyombo vya habari vina uwezo mkubwa wa kuweka na kuendeleza ajenda ya kimaendeleo. Lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ya pekee ya kiafrika inayokubalika na wengi barani Afrika kama lugha iliyo na uwezo wa kujenga undugu kati ya jamii mbalimbali. Hata hivyo, lugha na vyombo vya habari vinaweza kutumiwa vibaya na hivyo basi kuzua vita na kutokuelewana kati ya wanajamii mbalimbali. Tazama muziki unaochezwa katika vyombo vya habari; Wimbo ulioimbwa na ambao unawadhalilisha Wakamba na wimbo wa mwimbaji Turaco unaoongea juu ya deni la Wakikuyu kwa Wakalenjin.

Katika vyombo hivi vya habari, kuna vipindi ambapo wasikilizaji hupiga simu na kuchangia mijadala moja kwa moja na ambapo matamshi ya chuki hutolewa kupitia misemo, masihara, na methali zitumiazo lugha enyeji. Pia kunai ile hali ya kuwaruhusu wanasiasa kutoa matamshi ya uchochezi na chuki na

kutumia lugha isiyofaa katika vyombo vya habari. Kuzuka kwa vituo vya utangazaji vinavyotumia lugha enyeji (*FM stations*) kumechangia pakubwa matamshi ya chuki na uchochezi jamii mbalimbali za nchini Kenya. Pia kumezuka machapisho mengine ambayo husambaza habari zisizothibitishwa na ambazo huchangia kutokuaminiana na migogoro ya kijamii *(Alternative Press)*.

Je, simu za rununu na jumbe zinazotumwa kupitia mitandao ya kijamii (*Facebook, Twitter,* na hata *WhatsApp*) zimechangia nini katika kuleta uwiano na mshikamano? Wanasiasa wengi huwa na akaunti za *Twitter, Facebook*, na *WhatsApp* kusudi kuendeleza sera zao (siasa na maslahi yao).Kenya inawezaje kuthibiti mitandao ya kijamii? Jumbe zinazotumwa kupitia mitandao ya kijamii zinaweza kuwahamasisha watu kutenda maovu (Muluka & Nassiuma, 2017). Maendeleo ya kiteknolojia yanawafanya Wakenya kuwataka viongozi wa kisiasa kuwajibika katika kazi zao.

Vyombo vya habari vinaweza kutumiwa kuleta uwiano wa kijamii kwa njia zifuatazo: vitumiwe katika juhudi za kujenga umoja, uwiano na mshikamano wa kijamii, vihimize mazungumzo kati ya jamii zinazozozana, na viwe vinasisitiza maovu ya migogoro na kuonyesha watu njia inayofaa kufuatwa. Kuna matatizo mengi yanayovikumba vyombo vya habari katika juhudi za kujenga umoja, uwiano, na mshikamano.

Kwanza, viwango vya juu vya watu wasiojua kusoma na kuandikani tatizo ambalo haliwezi kushughulikiwa ipasavyo. Hapa Kenya, tunalo gazeti moja tu la kitaifa linalochapishwa kwa Kiswahili, **Taifa Leo**. Watu wengi wanaojua kusoma na kuandika hukimbilia kusoma magazeti ya Kiingereza. Ingefaa tujaribu kubadilisha mtindo na kuwamotisha watu wengi zaidi kusoma magazeti ya Kiswahili. Karatasi hii inahoji kuwa ingawa lugha ni chombo muhimu sana cha kuleta mshikamano na uwiano wa kitaifa, pia inaweza kutumiwa vibaya na hivyo basi kuzua vita na kutokueleanwa kati ya wanajamii mbalimbali. Sehemu ifuatayo inajadili uhusiano uliopo kati ya lugha, uwiano, na mshikamano wa kitaifa.

## Namna Vyombo vya Habari vinaweza kutumiwa kupunguza Uhasama na Migogoro

Licha ya kuwa vyombo vya habari vimechangia na vingali vinaendelea kuchangia uhasama na hivyo basi, kutinga uwiano na mshikamano wa kitaifa, vyombo hivi vinaweza kutumiwa kwa manufaa ya wanajamii na kuleta uwiano na mshikamano wa kitaifa bora tu vitumiwe kwa madhumuni na malengo yafaayo. Vyombo hivi vinaweza kutumiwa kwa njia zifuatazo ili kuleta uwiano na mshikamano wa kitaifa.

Kwanza kabisa, wanahabari wanapaswa kutangaza habari zisizoibua hisia na mihemko ya kisiasa inayoweza kusababisha migogoro. Mara nyingi wanahabari hutangaza habari ambazo kwa kiasi kikubwa huibua hisia na mihemko ya kisiasa

ambayo hutenganisha makundi mbalimbali katika jamii. Wanapaswa kusambaza habari sahihi na zisizopendelea upande wowote kati ya makundi hasimu. Endapo wanahabari watazingatia majukumu yao ipasavyo, watachangia katika kuleta uwiano na mshikamano wa kitaifa na kwa njia hiyo kuchangia katika kuharakisha maendeleo ya taifa.

Pili, wanahabari wanapaswa kujiepusha kutangaza habari ambazo hulenga kusifia na kutukuza uhasama baina ya wanajamii. Wanahabari wanapaswa kufichua chanzo na usuli wa migogoro wala sio kuelezea kinachotukia tu. Mara nyingi, vyombo vya habari huchukulia habari ambazo zinaonyesha tofauti za wanajamii badala ya zile zinazoonyesha na kusisitiza ushirikiano wa kijamii. Kadhalika, siku hizi, vyombo vya habari vimejaa habari zinazoonyesha uozo katika jamii; wizi, ubakaji, na mauaji ya wapendanao. Habari zinazopatikana katika vyombo vya habari hutamausha sana, kiasi cha kukuza migogoro zaidi baina ya wanajamii.

Tatu, ingekuwa bora iwapo vyombo vya habari vingewatambulisha wanaohusika katika migogoro. Wakati wanaohusika na mgogoro wowote ule wanapotambuliwa na wanahabari, uhasama huongezeka kati ya wahusika. Wanahabari wanafaa kujiepusha na suala la kuwatambulisha wahusika wa migogoro yoyote ile kwa lengo la kujiepusha na kupalilia uhasama wa kijamii.

Nne, wanahabari wanapaswa kujiepusha kutoa habari zisizo za ukweli. Mara nyingi tumeshuhudia wanahabari wakitoa habari ambazo hazijathibitishwa na ambazo huenda hazina ukweli wowote. Habari za aina hii zinaweza kuchangia uhasama baina ya wanajamii. Kwa hivyo, ni jambo la busara wanahabari wakijiepusha na kueneza habari ambazo hazijathibitishwa na ambazo huenda ni uvumi tu.

Tano, hata pale ambapo habari ni za ukweli, wanahabari wanapaswa kujiepusha kutilia chumvi habari zinazoweza kuzua uhasama. Makampuni mengi ya utangazaji siku hizi yanaongozwa na kutawaliwa na hamu ya kuwa na mauzo mengi. Mauzo hayo hupatikana tu iwapo habari zilizomo katika vyombo hivyo ni za kuvutia. Kwa hivyo kuna ushindani mkubwa sana unaoendelea kati ya makampuni ya habari na utangazaji, ushindani unaowezeshwa zaidi na utiaji chumvi wa habari.

Sita, pale ambapo kuna makundi mawili hasimu, wanahabari wanapaswa kujiepusha kupendelea kundi lolote lile. Wanahabari wanapaswa kuhimiza umoja na uwiano wa kitaifa na bara zima la Afrika. Iwapo wanahabari watalipendelea kundi moja kati ya makundi hasimu, basi uhasama utapaliliwa zaidi na hivyo basi, uwiano na mshikamano kutingishika.

Hatimaye, wanahabari wanapaswa kujiepusha na tabia ya kupendelea kutangaza matokeo ya uhasama na migogoro, jambo ambalo linaweza kupatia makundi haramu (kama vile Al Shabaab) umaarufu wautamanio. Utangazaji wa

aina hii hupelekea wananchi watiifu kukata tamaa maishani. Wanapaswa kuweka na kuzingatia ajenda za kimaendeleo kwa kusisitiza mambo yanayounganisha watu kuliko yale yanayowatenganisha. Wanahabari wanapaswa kuhimiza na kusambaza sanaa, fasihi, muziki, na kazi za kubuni na za kitamaduni. Kwa njia hii watakuwa wanasaidia kujenga uwiano, umoja na mshikamano.

Uwiano na mshikamano unahitaji juhudi za kila mmoja wetu. Tunaweza kuchangia kwa njia gani katika kuleta uwiano na mshikamano wa kijamii hapa Afrika? Yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo yanayoweza kusaidia kujenga uwiano na mshikamano. Matamshi ya uchochezi yanaweza kuathiri pakubwa maendeleo ya kitaifa na bara zima la Afrika kwa jumla katika nyanja za kijamii, kiuchumi, na kisiasa (Muluka na Nassiuma, 2017). Ili kuweza kudhibiti matamshi ya chuki ambayo huchangia kuvuruga uwiano na mshikamano, kuna haja ya kuelezea ni nini kinachoweza kuchukuliwa kuwa matamshi ya uchochezi. Mara nyingi wanasiasa huchochea hisia za chuki lakini wanapokaripiwa, huwa wanajificha katika usemi kuwa waliripotiwa kimakosa.

Kuna haja ya kuhakikisha kuwa watu wanaolengwa na wanasiasa wachochezi wanalindwa kikatiba na kisheria na serikali. Wananchi wa kawaida ndio wanaotaabika zaidi kutokana na matamshi ya chuki. Ili kuhakikisha kuwa watu hawa hawataendelea kutaabishwa na wale wanaowatesa, ingefaa serikali iwalinde na kuwapa ulinzi wa kutosha kila wakati. Aidha, ipo haja ya kuhakikisha kuwa wale wanaotoa matamshi ya uchochezi wanakabiliwa vilivyo kisheria na kulipia makosa yao bila kujali nyadhifa zao katika jamii. Sheria inafaa itumiwe kwa watu wote kisawasawa. Aidha, sheria zifaazo zinafaa kuundwa uli kukabili matamshi ya uchochezi. Hali ilivyo sasa ni kwamba sheria zilizoko hazimlindi mtu wa kawaida ila zinawalinda wenye uwezo ambao pia huwa na uwezo wa kuwalipa wanasheria watajika. Kuna haja ya kuhakikisha kuwa kuna usawa na haki katika ugavi wa nyadhifa za uongozi na rasilmali ya taifa ili kusiwe na jamii inayohisi kuwa imetengwa.

Ni muhimu kushughulikia masuala ya haki za kibinadamu zilizowahi kutokea siku za nyuma na vilevile kuwaridhia wale ambao haki zao zilikiukwa. Kuna haja ya kuhakikisha kuwa wanahabari wanapata masomo na stadi zinazofaa katika kazi ya uanahabari. Pia serikali inaweza kutenga pesa kwa ajili ya kuboresha masomo ya uanahabari. Ili kupunguza athari za semi za chuki, kuna haja ya kuwashirikisha vijana katika juhudi za kuleta amani na maridhiano ili wawe na uelewa unaofaa wa siasa za nchi zao. Kuna haja ya serikali, bunge na hata mahakama kushirikiana katika vita dhidhi ya uchochezi na wasaidie kuponya vidonda vya uchochezi. Kuna haja ya kuzuia matamshi yaliyokaririwa *(stereotypes)* na yasiyo na uasili wowote kuhusu jamii zingine. Kuna haja ya wanahabari kupata ujuzi wa kuripoti kuhusu migogoro *(conflict reporting)* na wafuate maadili ya uanahabari wanapoendesha kazi yao ya uanahabari.

## Hitimisho

Lugha huwa na nafasi kubwa sana katika kuchangia uwiano na mshikamano wa kijamii. Hatuwezi kupata uwiano na mshikamano iwapo kwanza hatuna lugha mawasiliano ambayo itayawezesha mawasiliano baina yetu na pili lugha hiyo iwe inatumiwa kwa njia zifaazo. Makala haya yameonyesha kuwa ili kushughulikia suala la uwiano na mshikamano wa kitaifa na wa bara zima la Afrika, ni sharti watumiaji lugha (hususan wanasiasa na watu wengineo walio na uwezo mkubwa katika jamii) watumie lugha kwa namna ambayo itasaidia kuleta uwiano na mshikamano badala ya kuleta utengano na kuzua migogoro na uhasama. Vile vile imeonyeshwa kuwa vyombo vya habari vina umuhimu sana katika ujenzi wa uwiano na mshikamano na hivyo basi inafaa vishirikishwe katika juhudi za kuleta na kuendeleza amani. Kadhalika, imeonyeshwa kuwa ili juhudi za kuleta uwiano na mshikamano ziweze kufanikiwa, kuna haja ya kushirikisha pande zote za utawala: serikali, bunge na idara ya mahakama. Kupitia ushirikiano wa pande zote hizi tunaweza kutunga sheria zifaazo, kutekeleza sheria hizo na kuhakikisha kuwa sheria zinafuatwa na kila mtu anayehusika na uwiano na mshikamano. Hali kadhalika vijana kama kizazi cha siku zizajo wanafaa kushirikishwa katika juhudi zozote zile za kuleta uwiano na mshikamano wa kitaifa, kikanda, na wa bara zima la Afrika.

## Marejeleo


Arif, M. S., Mahmood, M. A., & Mahmood, C. R. (2011). Diversity and variation in Pakistani English. *Journal of Social Sciences, Vol. 4 No. 2, August 2011*: 131-139.

Ayeomoni, M. O. (2011). Languages and domains: Nigerian situations. *Journal of Social Sciences, Vol. 4 No 2, August 2011*. 141-155.

Guyo, A. G. (2013). The role of mass media in promoting national cohesion: A case study of Marsabit County. Unpublished MA Dissertation. University of Nairobi.

Jabbar, J. (2013). Role of media in national development in the 21st century. *Criterion Quarterly, Vol. 2 No 2. October 2013*. 1-11.

Kiango, J. G. (2002). Nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa jamii mpya ya Afrika Mashariki. *Nordic Journal of African Studies 11(2)*: 185-197.

Mann, C. C. (2011). Language, mass communication and national development: the role, perceptions and potential of Anglo-Nigerian Pidgin in the Nigerian mass media. Paper presented at the International conference on language in development (3rd Langkawa, Malaysia. July 29-31, 1997.

Melkote, S. (2003). Mass media in support of sustainable development. *Knowledge for sustainable development: An insight into the Encyclopedia of Life Support Systems. Vol. 1*. UNESCO/EOLSS. 2003 (www.eolss.net)

Mirembo, E. K. (2015). The role of the media in political conflict resolution: An analysis of the Saba Saba rally in Kenya. Unpublished MA Dissertation. University of Nairobi.

Mulokozi, M. M. (2002). Kiswahili as a national and international language. Paper presented at the University of Helsinki symposium. Available at http://www.helsinki.fi/hum/aakk/documents/kiswahili.pdf

Muluka, S., & Nassiuma, B. K. (2017). Hate speech: A derivative of Kenyan politics. *International Journal of Communication and Public Relations. Vol. 2. Issue 2 No 4. 2017*: 55-69.

Ogola, G. (2011). The political economy of the media in Kenya: from Kenyatta's nation-building press to Kibaki's local-language FM radio. *Africa Today 57(3)*. Accessed through Project Muse: Today's research, tomorrow's inspiration. http:muse.jhu.edu. Access provided by University of Central Lancashire on 09/28/2011 at 9.37 a.m. GMT.